**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA - MIKINDANI**

**Kumb. Na.MM/MC/S.2/70/VOL1/138** **27 JUNI, 2025**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Halmashauri ya Manispaa Mtwara-Mikindani kupitia kibali cha ajira mpya chenye **kumb. Na. FA.97/228/01/A/25** cha tarehe **29 Aprili, 2025** chenye kada ya Dereva Daraja la II nafasi (9) kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hivyo Mkurugenzi wa Manispaa Mtwara-Mkindani anawatangaza nafasi za kazi na anakaribisha maombi kwa watanzania wote wenye sifa za kujaza nafasi hizo kama iliyoainishwa hapo chini.

## 1.0 DEREVA DARAJA LA II - NAFASI- 9

### 1.1.1 KAZI/ MAJUKUMU YA DEREVA

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari;
ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi;
iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari;
iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali;
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari;
vi. Kufanya usafi wa gari; na
vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

### 1.1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na Leseni ya Daraja E au C ya uendeshaji magari ambayo wamefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa, Manispaa ya Mtwara - Mikindani, S.L.P 92, 12 Barabara ya Tanu, 63182 Mtwara. Simu: +255 232333102, Nukushi +255 23 2334794 Baruapepe: md@mtwaramikindanimc.*go.tz* Tovuti: www.mtwaramikindanimc.go.tz

mmoja (1) bila kusababisha ajali pamoja na vyeti vya mafunzo vilivyowapatia sifa ya kupata madaraja husika. Wawe wamehudhuria mafunzo ya msingi ya Uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha VETA au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

### 1.1.3 MSHAHARA

Ngazi ya Mshahara ni TGS B1.

### MASHARTI YA JUMLA

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania, wenye umri wa kuanzia miaka18 na usiozidi miaka 45.

ii. Waombaji waambatanishe Cheti cha Kuzaliwa,

iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye Anuani, Namba za Simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) wa kuaminika,

iv. Waombaji wote waweke nakala za vyeti vya taaluma na vyeti vya Kidato cha Nne na Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika kwenye ***Ajira Portal,***

v. ***Testimonials "Provision Results", "Statement of Results" Hati ya Matokeo ya Kidato cha Nne na Sita HAVIKUBALIKI,***

vi. Waombaji kazi wa kada ya Dereva II wenye leseni Daraja E au C wanapaswa **KUAMBATISHA** vyeti vya mafunzo ya Udereva vilivyowapatia sifa ya kupata madaraja husika

vii. Waombaji wote waweke picha mbili *"Passport Size"* ya hivi karibuni katika ukurasa wa *Ajira Portal,*

viii. Waombaji waliosoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vinahakikiwa na kuthibitishwa na mamlaka husika yaani TCU, NECTA na NACTE,

ix. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi,

x. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko

katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka wenye **Kumb. Na. CAC.45/257/01/D/140** wa tarehe **30 Novemba, 2010.**

xi. Uwasilishwaji taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria,

xii. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **10 Julai, 2025,**

xiii. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya Elimu, Anuani ya barua hiyo ielekeze kwa

**Mkurugenzi wa Manispaa,**
**Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani,**
**12 Barabara ya TANU,**
**S.L.P 92,**
**63182 MTWARA.**

xiv. **MUHIMU: Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira kupitia anwani ifuatayo; https://portal.ajira.go.tz/ (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa ('Recruitment Portal')**

xv. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili
HAYATAFIKIRIWA.

Tangazo hili limetolewa na;

MKURUGENZI WA MANISPAA
MTWARA - MIKINDANI
S. L. P. 92
MTWARA

Mwl. Hassani B. Nyange
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**MTWARA - MIKINDANI**